


# IMANI NDIYO USHINDI WETU

 Ni majaliwa kuwa hapa usiku wa leo katika huduma ya Bwana. Lakini bila shaka ni jambo la kusikitisha kwamba watu hawawezi kupata nafasi ya kuketi, baada ya sisi kuwaalika waje, halafu hakuna mahali pa kuketi. Nami nilipokuwa nikipanda kuja, sasa hivi, mbona, kulikuwa na watu kwenye madirisha, na huku na huko mitaani, na kadhalika. Wala hakuna—hakuna hata nafasi kwa ajili yao ku- . . . kuingia jengoni. Lakini ni kanisa dogo tu.

<sup>2</sup> Kamwe hatuutangazi. Na hata kwenye gazeti hapa, tunaninii tu. . . Loo, baadhi ya marafiki zetu wakipiga simu, wakizungumza kuhusu kuja kuombewa. Nasi tuliwambia waje tu. Kwa hiyo habari zinaanza kuenea tu polepole kote, mtu fulani alikuja kutoka Louisville, kisha anamwambia mtu mwingine, na mtu mwingine. Mnajua, ndivyo inavyoenea.

<sup>3</sup> Nilitaka kuchukua shule ya upili hapa chini. Lakini wao. . . Sikuweza kuipata kwa sababu shule inaendelea. Au, basi tungeitangaza. Nataka watu, wenyeji wajue kuwa hatukuwa tukijaribu kuwasukuma mbali nao, lakini tulijua tu hicho chumba kilikuwa kibaya sana. Kwa hiyo sisi, kama tungeweza kuipata hiyo shule ya upili, tungefanya hivyo, lakini hatungeweza.

<sup>4</sup> Kwa hiyo, sasa, usiku wa leo utakuwa ndio usiku wa mwisho kwa vile vitabu huko nyuma, alivyo navyo Bw. Mercier na hao wengine hapa, na kanda na kadhalika.

<sup>5</sup> Na halafu kesho asubuhi ni shule ya Jumapili. Na mara baada ya shule ya Jumapili kuchukua mahali pao, Bwana akipenda, ninataka kuzungumza juu ya mahubiri ya uinjilisti, kesho asubuhi. Hiyo itaanza saa tatu na nusu, nafikiri, sivyo, Ndugu Neville? Saa tatu na nusu, shule ya Jumapili inaanza. Na mara baada ya masomo ya shule ya Jumapili, tunataka kuzungumzia somo la—la ujumbe wa kiinjilisti, wito kwa mwenye dhambi. Na siku hizi usiku zaidi sana tumekuwa tukiutoa, tangu Jumapili iliyopita usiku, kwa ajili ya wagonjwa na wahitaji, wanaoteseka.

<sup>6</sup> Halafu basi, kesho usiku, tutajaribu, kama kweli tunaweza, kwa njia yoyote, kuchukua kadi zote za maombi ambazo zimesambazwa, kwamba kila mtu ambaye amekuwa na kuchukua kadi za maombi, sisi. . . baada ya ujumbe kwisha, ikiwa itabidi tuwaache wengine warudi, na kisha kuwaleta hao wengine, ili tuweze kuendeleza mstari wa maombi, tutafurahia kufanya hivyo.

<sup>7</sup> Na kadi za maombi za kesho usiku zitatolewa baada ya shule ya Jumapili asubuhi. Mara tu baada ya shule ya Jumapili,

iwe yapata, labda, saa tano na nusu, ka—kadi za maombi zitatolewa, kesho. Kwa hiyo ninyi mlio na wapendwa wenu, na kadhalika, wanaokuja kuombewa, mbona, acheni wawe hapa yapata, angalau saa tano na nusu, kama hawawezi kuwepo kwa ajili ya Ujumbe wa asubuhi.

<sup>8</sup> Hiyo ni kusema, ikiwa una ma—mahali pa ibada, ambapo umekuwa ukihudhuria, mbona, tu—tusingekuondoa hapo hata kidogo. Tungetaka tu ujisikie huru kabisa kuhusu kile ambacho ungefanya.

<sup>9</sup> Nimekuwa na shughuli nyingi sana leo. Na dakika chache tu zilizopita, walikuja, kasema, “Vema, ukishuka chini, unaweza kuanza kuhubiri sasa hivi.” Ilikuwa, tayari, ile maskani ndogo ilikuwa imejaa. Kwa hiyo niliwazia tu juu ya vifungu vichache ambavyo nilifikiri ningezungumzia, usiku wa leo.

<sup>10</sup> Nami ninataka kumshukuru Bwana, kwanza, kwa yote ambayo ametufanyia. Taarifa hizo zikirudi kutoka kwa wale ambao wameombewa, na wamekuwa mkutanoni. Mambo makubwa yamefanyika, kwa ajili tu ya mahali hapa padogo. Na si zaidi ya kwamba wanapaswa kuja hapa juu na kuombewa kibinafsi, lakini inaonekana kwamba watu huko nyuma katika kusanyiko wanaupata vizuri zaidi kuliko wanavyoupata hapa jukwaani. Kwa hivyo tunafurahia hilo. Hilo ni zuri sana, kuwaona wakiupata namna hiyo.

<sup>11</sup> Sasa, usiku wa leo, nimechagua kwa ajili ya somo: *Imani Ndiyo Ushindi Wetu*. Nami ningependa kusoma sehemu ya Maandiko yanayopatikana katika Yohana wa Kwanza, mlango wa 5 na kifungu cha 4.

*Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu: na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu.*

<sup>12</sup> Sasa, Maneno ya ajabu sana! Imani yetu ndiyo ushindi. Na sasa, tunazungumza juu ya ushindi. Kumekuwa na ushindi mwingi mkubwa uliopatikana katika kipindi hiki kirefu cha miaka ambacho binadamu wamekuwa duniani.

<sup>13</sup> Nilikuwa nikisoma kitabu juu ya kujisalimisha kwa—kwa Paris, ambapo, katika hivi vya mwisho, ama Vita vya Pili vya Dunia, ambapo Hitler alikuwa ameletwa Paris, kwenye ule Mnara wa Ushindi, wanasema kuwa ulikuwa ni ushindi mkuu sana hata ilichukua saa kadhaa kwa askari hao wa Kijerumani kwenda taratibu bila kukunja magoti moja kwa moja kupitia kwenye Mnara wa Ushindi. Wakati Hitler aliposimama miguu sawa na hewa yote ilikuwa nyeusi, juu, anga zilifunikwa, kutokana na kupita kwa ndege. Wakati mkuu sana wa ushindi, kwamba baada ya wao kushinda vita dhidi ya Ufaransa, na Ufaransa ilikuwa imejisalimisha kwa Ujerumani.

<sup>14</sup> Halafu huko London, Uingereza, nilipata fursa wakati mmoja ya kuona huko, kwenye lile kongamano, picha ya sinema

ya mahali ambapo...Ilikuwa imepigwa na Warusi, wakati Berlin ilipojisalimisha kwa Urusi. Na jinsi ambavyo ule wingi mkubwa mno wa vifaa vya kijeshi, mizinga hiyo mikubwa waliyokuwa nayo kwenye...iliyowekwa kwenye mizinga hii mikubwa ambayo ingeweza kuzunguka; ndio kwanza iingie Berlin. Ingekuwa vigumu kwako kuona jinsi uhai wowote ungeweza kuwepo. Kwa maili baada ya maili, na kila mtu akipiga risasi kwa usahihi, kufikia ambapo wanakuja tu kama kundi kubwa la nzige. Nao kwa urahisi wakaupondaponda tu Berlin wakauangamiza.

<sup>15</sup> Na wakati, basi, waliviondoa vifaru vyao nao a—askari wa miguu wakaingia ndani na kuamalizia, wakaagizia na kumleta Bw. Stalin. Nao walipomleta, kwa ndege, nayo ikatua, askari hao wote wa Kirusi walishuka barabarani, kama msokoto ule na hatua wapigazo, kama mshindi, ishara ya mshindi ya Urusi. Na jinsi Stalin alivyosimama miguu sawa wakati makumi ya maelfu ya askari walitembea taratibu kwenye mitaa ya Berlin, ulipokuwa majivu. Na wakati wanawake wa Kijerumani walikuwa wamebakwa mitaani, nao watoto, wakauawa, na baadhi yao wakachomwa moto, na kadhalika, lakini huo ulikuwa ni ushindi mkuu kwa Urusi.

<sup>16</sup> Kisha ninaambiwa kwamba Napoleon, yule mshindi mkuu wa siku zilizopita...Miaka kadhaa iliyopita, yapata miaka mitano, nilipata fursa ya kusimama karibu na Waterloo. Nami nilikuwa...nilichukua kitabu kidogo pale, na nilikuwa nikisoma maisha ya Napoleon. Aliwachukia Wafaransa. Alikuwa Ufaransa, akiwa amezaliwa huko kisiwani, kisha akaja Ufaransa kujilipizia kisasi kwao, bali akawa mshindi mkuu. Alikuwa muungwana, kwanza kabisa. Lakini mafanikio yakaingia kichwani mwake.

<sup>17</sup> Ndipo inasemekana kwamba wanawake, walipokuwa wakienda kuwalaza watoto wao wachanga kitandani, kwamba aligopwa sana...Aliua kila kitu ambacho hakikukubaliana naye. Hata, wanawake, badala ya kusema, “Zimwi litakushika,” wangesema, “Napoleon atakushika.” Nao hao maskini jamaa wenye macho maangavu wangevifunika vichwa vyao, haraka sana, wakiwazia juu ya lile zimwi kubwa Napoleon.

<sup>18</sup> Lakini, mnaona, ushindi ambao alishinda haukudumu. Alikuwa mkataza pombe, kwanza kabisa, kisha akafa akiwa na umri wa miaka thelathini na mitatu, mlevi sugu.

<sup>19</sup> Ushindi wa aina hiyo haudumu, kwa sababu hauna msingi mzuri. Kamwe huwezi kupata mema kutoka kwa mabaya. Huna budi kutumia kanuni za mambo vizuri.

<sup>20</sup> Na yeyote wenu anajua, kwamba katika Olimpiki au mazoezi yoyote ya riadha, haijalishi kama umekuwa wa kwanza kufika kwenye mashindano, lakini ikiwa hujaucheza huo mchezo

kulingana na sheria, unaondolewa. Huna budi kutumia sheria ipasavyo.

21 Na hivyo ndivyo ilivyo kwa maisha ya mwanadamu. Huwezi kutumia kanuni za mchezo wa maisha vibaya na kutarajia kushinda. Huna budi kuucheza kulingana na Neno la Mungu na kusudi ambalo uliletewa hapa.

22 Sasa, kuna watu wengi sana ambao hawaonekani kuwa na namna yoyote ya kusudi maishani, hasa katika siku hii tunayoishi sasa. Watu wanaonekana tu kufikiria kwamba wanachopaswa kufanya ni kushindana na mtu mwingine, kwa mitindo ya ulimwengu, na kwa vishawishi ambavyo ulimwengu umewapa.

23 Hivi tu, kama ukienda shuleni na baadhi ya wasichana wadogo wanavaa gauni dogo, au vazi fulani, ama chochote ungliita, shauku zote wengine wote shuleni walizo nazo ni kumwiga msichana huyo. Baadhi ya wanawake wanaona kwenye televisheni mama fulani akitoka, na amevaa mtindo fulani, vema, hiyo ndiyo shauku yao ni kuvaa na kutenda hivyo. Na hiyo inaonekana kuwa karibu ndiyo kikomo cha shauku za Marekani, ni kupata kazi mpya, au kupata nyongeza ya mshahara wako, na kununua televisheni, au gari jipya.

24 Hebu niseme hivi. Mambo hayo yanaweza kuwa sawa, lakini kuna shauku kuu zaidi katika maisha ya mwanadamu kuliko mambo hayo. Nao Wakristo wanapaswa kuweka shauku kwenye matamaniao ya juu zaidi.

25 Nafikiri itatufaidi sisi sote kuketi chini na kujiuliza kwa nini tuko hapa, kwanza kabisa. Na yeyote Yule ambaye alikuwa mwema vya kutosha kutuleta hapa, inatupasa tutafakari na kumwuliza Yeye angetutaka tufanye nini, kusudi la sisi kuja, kutimiza yale aliyotukusudia. Lakini inaonekana kuwa tunataka tu kushindana na ulimwengu.

26 Sasa, Biblia ilisema kwamba tunaweza kuushinda ulimwengu. Basi tunaushindaje? Sio kwa kuendana na mitindo ya ulimwengu. Lakini Biblia ilisema kwamba imani ni ushindi unaoushinda ulimwengu.

27 Inanikumbusha wakati mmoja ambapo ninii... Sipendi kusema neno hili, lakini ilikuwa tu ni ombaomba aliyekuja mlangoni. Naye akasema, "Unaweza kunipa sa—sambusa?"

28 Nikasema, "Hakika. Je, waweza kuingia ndani?" Na badala ya kumwandalia sambusa, niliwazia ningempikia chakula. Basi nikampikia karibu kile ningeweza kumpikia mahali pale, ndipo nikamketisha ale. Basi alipokuwa anakula, nilifikiri ningezungumza naye, kwa kuwa niliona alikuwa m—msafiri. Nami nikasema, "Umetoka wapi?"

29 Akainua tu mabega yake kidogo, na kusema, "Sikutoka popote."

Nikasema, “Basi unakwenda wapi?”

<sup>30</sup> Ndipo akaacha kula, akanitazama, akasema, “Siendi popote.” Akatazama pande zote na kumeza funda kubwa, akasema, “Bwana, mahali ambapo kofia yangu inatulia, ndipo ninapotulia mimi.”

Nikasema, “Kumbe.” Nikasema, “Umekuwa ukifanya hivi kwa muda gani?”

<sup>31</sup> Akasema, “Loo, miaka ishirini, au zaidi.” Bila shauku ya ku—kujiboresha!

<sup>32</sup> Sasa, huo karibu tu ndio msimamo wa watu. Ninachokiita tu “wazururaji, watangitangi.” Nao watu wanaojiunga na kanisa karibu wako hivyo. Mara nyingi nimefikiria juu ya “mbao zinazopwelewa, zinazochukuliwa na maji.” Ubao unaopwelewa, huning’inia tu kwenye kila namna ya takataka. Hivyo ni karibu vile watangitangi wafanyavyo kanisani ama mahali popote.

<sup>33</sup> Sasa hebu chukua kijito, kama kijito cha maisha, na mbao nyingi sana zinazopwelewa zikining’inia kwenye kila lundo la takataka. Na, hata hivyo, mashua inakuja, iliyotengenezwa kwa mbao, pia. Lakini ukiangalia, hizo mbao zimetengenezwa na kuchongwa na bingwa ambaye amejenga hiyo mashua. Si kwamba tu imechongwa, bali inaongozwa na nahodha, na inasukumwa na nguvu fulani.

<sup>34</sup> Na sote tumeumbwa kwa vitu vile vile. Inategemea tu kule shauku yako imeelekezwa. Je, uko tayari kuruhusu Fundi mkuu atengeneze, kutoka kwako, kile ambacho angeweza kutumia, na kile ambacho angeweza kudhibiti, na kile ambacho angeweza kutia nguvu?

<sup>35</sup> Kama maskini chombo hiki ambacho kimefanywa tofauti, na kimeundwa na mkono wa fundi mkuu, kamwe kikikwama kwenye magugu katika maji ya kina kifupi, kuna nguvu nyuma yake, bali ndogo ambayo bwana anaweza kufungulia, na kukisukumia kwenye kina kirefu cha maji tena.

<sup>36</sup> Mungu anataka kutufinyanga na kutufanya vile anavyotaka tuwe. Lakini tunawezaje kufanya hivyo, au Mungu anawezaje kufanya hivyo, wakati hata hatutasimama kimya apate kufanya jambo hilo? Tunataka kujiongoza wenyewe. Tunataka kuwazia kwa njia yetu ya kuwazia.

<sup>37</sup> Na watu wengi huja kanisani, na kujiunga na kanisa, na kuweka jina lao kwenye kitabu, na hata hawazingatii kile kanisa hilo linaamini, ama kulichunguza kanisa hilo, jinsi wanavyohubiri Neno la Mungu, ama kama wanaitetea Injili kamili ama la, ama wanachagua tu sehemu moja na kuongeza kanuni ya imani. Kuelea, kuzurura, kamwe hutaweza kuwa chochote.

<sup>38</sup> Lakini hebu niwaambie jambo fulani, usiku wa leo, ninyi mlio ndani na nje ya jengo hili. Utaishia kwenye kikomo fulani

moja ya siku hizi, ambacho kitakuwa katika bonde la uvuli wa mauti. Ningekushauri kwenye saa hii, ujiandae kukutana na Mungu ambaye itambidi akutane nawe saa hiyo. Utakutana Naye ama kama kipeo ambacho Yeye amekifanyia kazi, au kipande kinachoelea cha ubao unaopwelewa kwenda kwenye kikomo chako cha mwisho. Kwa hivyo usitumie maisha haya kuzurura tu, na kuelea huku na huku, na—na kupata kazi bora zaidi, na kuvaa vizuri zaidi, na kupata televisheni mpya, ama—ama gari bora zaidi. Maisha yanamaanisha zaidi ya hayo. Usijaribu kuyatumia kusema tu, “Vema, kama hao wengine wakijiunga na kanisa, nami nitajiunga, pia.”

<sup>39</sup> Unapojiunga na kanisa, unapaswa kwanza kutafuta, na kujua kanisa hilo linasimamia nini. Je, ni mahali tu ambapo watu hukusanyika pamoja kwa ajili ya ushirika? Au, je, ni mahali ambapo panahubiri Neno la Mungu aliye hai, na kutetea kila kanuni aliyoifia Yesu? Unapaswa kufanya hivyo. Usielee tu ndani na kuchukuliwa na mkondo. Kwa sababu, “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo Uzimani, na lakini ni wachache watakaolingia mle ndani.” Kwa sababu, “Njia ni pana iendayo upotevuni, na wengi wataingia mle.”

Hatuna budi kuwa na kusudi la jambo fulani.

<sup>40</sup> Sasa, haikuwa hivyo katika siku zilizopita, ama katika siku hizi, ambapo wakati mtu alipomjia Mungu, alikuwa na kusudi la kufanya hivyo. Kama kusudi lako ni kutangatanga tu na kusanyiko hilo, au ni kutazama juu kwa Mungu?

<sup>41</sup> Danieli, alipopelekwa huko Babeli, ingawa alikuwa akihama nyumbani kwake, na ilimbidi awe mtumwa wa taifa lingine la watu, lakini Danieli aliazimu moyoni mwake, haijalishi walimfanyia nini, hatajitia najisi kwa dhambi ya Babeli.

<sup>42</sup> Loo, laiti tungalikuwa na watu hodari zaidi kama hao, ambao wangeazimu moyoni mwako, “Kama mimi ni Mkristo, nitatafuta kila baraka ya Kiungu ambayo ni mali yangu, na kuidai. Ikiwa Biblia inafundisha kwamba ninaweza kumpokea Roho Mtakatifu, nitakaa magotini mwangu mpaka Mungu anipe Roho Mtakatifu, na nisitangatange tu.”

<sup>43</sup> Nilikuwa nikisoma hadithi ya maisha ya maskini Mjomba Buddy Robinson muda fulani uliopita. Naye alikuwa mtu mashuhuri sana, na m—mtu mwenye upendo, na mtu wa imani. Naye akaanza kumwonea njaa Roho Mtakatifu, kwa sababu Biblia ilifundisha hayo. Basi inasemekana siku moja alikuwa akilima mahindi. Naye akamsimamisha nyumbu wake mzee, Alex, akapiga magoti kwenye safu ya mahindi na kusema, “Mungu, usiponipa ubatizo wa Roho Mtakatifu, utakaporudi duniani utakuta mifupa yangu imelala papa hapa.” Hiyo ni kuazimu moyoni mwako. Hiyo ni kuwa makini kweli.

<sup>44</sup> Unapopata azma ya namna hiyo moyoni mwako, Mungu atafungua madirisha ya Mbinguni. Jambo fulani halina budi

kutukia. Huna budi kuwa makini na Mungu, na kuwa na azma fulani, na shukrani kwa ajili Yake kukuokoa.

<sup>45</sup> Basi Danieli alipokwisha kuazimu moyoni mwake, naye ibilisi akamfanya kuthibitisha hilo, lakini tunaona ya kwamba ilitahimili mbele ya simba mwenye njaa.

<sup>46</sup> Na mtu anayewahi kumjia Mungu na kweli, chini moyoni mwake, anapata imani iliyotulia, itastahimili katika kinywa cha mauti, au katika kinywa cha ugonjwa, katika kinywa cha huzuni. Itastahimili, kwa maana imani ni ushindi. Umeshinda kwa imani yako.

<sup>47</sup> Ibrahimu, mtu tu asiye na kusudi maalum maishani mwake, akiwa tu na baba yake na marafiki zake, wakishuka kutoka Babeli. Wakakaa katika Shinari, na hapo wakajenga mnara, na kadhalika. Na wao. . .

<sup>48</sup> Siku moja, Ibrahimu alipokuwa akiomba, hapana shaka, aliomba kwa bidii, mpaka akaushika mkono wa Mungu. Alifanyaje jambo hilo? Kwa imani. Labda aliwazia hivi, “Kama kuna Mungu aliyeijenga safina, na kumwacha Nuhu aelele juu yake, Yeye angali hai leo.” Mahali fulani katika nchi ya wapagani, ambako alikuwa a—akikaa, aliugusa mkono wa Mungu. Na mle ndani, Mungu akampa ufunuo ya kwamba kulikuwako na Mji Ambao Mwenye Kuubuni na Kuujenga alikuwa ni Mungu.

<sup>49</sup> Nasi tunasoma ya kwamba, maishani mwote mwa Ibrahimu, alikuwa msafiri na mgeni kwa ulimwengu, kwa kuwa shauku yake moja ilikuwa ni kuupata Mji ule Ambao Mwenye Kuubuni na Kuujenga alikuwa ni Mungu. Aligusa kitu. Alimshika Mungu, na imani katika Mungu huyo, hata akatangulia kuuona Yerusalemu Mpya. Naye akaweka mzigo wake mgongoni akawa mzururaji. Sio kutangatanga tu, bila azma yoyote; alikuwa na imani ya kwamba kulikuwa na Mji Ambao Mwenye Kuubuni na Kuujenga alikuwa ni Mungu, Mji wa Milele. Alikuwa na kusudi maishani, kupaona mahali hapo.

<sup>50</sup> Naomba niseme hapa, ya kwamba, siku moja wakati vita vilipokwisha, alikutana na Mfalme wa Mji huo. Naye akampa ushirika, mkate na divai; Melkisedeki.

<sup>51</sup> Loo, huwezi kuazimia chochote cha ahadi ya Mungu, moyoni mwako, pasipo kupata uhalisi wake. Ikiwa nafsi yako imeteswa na dhambi na mashaka, na misukosuko na kuvunjika moyo, na kuna kitu ndani yako ambacho kinakwambia kuwa kuna mahali unapoweza kushinda hayo, mbona basi unatangatanga kutoka kanisa hadi kanisa na kutoka mahali hadi mahali? Piga magoti tu mpaka utakapoigusa Mbingu.

<sup>52</sup> Na kama nilivyosema jana usiku, nenda kupita vizuizi vya sauti, ndipo utapata kusudi la maisha. Utakuwa na kusudi la kuwa mfuasi wa kanisa. Utakuwa na kusudi la kubatizwa. Utakuwa na kusudi katika kile unachotafuta. Maana, tunajua

ya kwamba Mungu ni mwaminifu, na Mungu ni wa kweli, na Mungu hawezi kusema uongo.

<sup>53</sup> Na kama Mungu aliliweka hilo moyoni mwa Ibrahimu, kwa Sauti Yake, Neno Lake, basi Mungu ameliweka ndani, mbele yetu, katika Biblia Yake, na kwa ushuhuda wa Roho Mtakatifu, kwa kurudi kwa Roho Mtakatifu katika ishara na maajabu, kwamba Yesu Kristo angali hai, na ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Basi kwa nini tutafute tena yale mambo tunayotamani?

<sup>54</sup> Kama unahitaji, haja yoyote, lolote ambalo Mungu ameahidi katika Biblia Yake, Yeye yuko hapa usiku wa leo kutimiza haja hiyo. Hakuna haja ya kutafuta mbali zaidi. Uwepo Wake upo hapa. Roho Yake iko hapa. Naye anapenda, na yuko tayari, na anatamani kukupa kile unachotafuta sana. Kwa nini usubiri tena?

<sup>55</sup> Unapomjia, usije kama mzururaji, “Nitaenda huko nijaribu nione kama inafanya kazi.” Kamwe hutafika popote.

<sup>56</sup> Lakini, unapokuja na azimio la namna hii, kwamba umejitolea kabisa, kwa hali na mali; wakati umechoka na ulimwengu, na dhambi, na kutokuamini, na kuvunjika moyo, na mashaka, na umjie Mungu aliye hai, pamoja na nanga iliyofungwa imara katika Mwamba wa Miaka; Roho Mtakatifu yuko hapa kukuvuta akuingize katika Uwepo wa Mungu aliye hai, ambao utakupa imani ambayo itashinda chochote kilichoko ulimwenguni, maradhi, magonjwa, na hata kifo chenyewe.

<sup>57</sup> Unasema, “Ulisema ‘kifo,’ Ndugu Branham.” Na hicho ndicho nilichomaanisha: kifo.

<sup>58</sup> Je, si Lazaro ndiye aliyekuwa amelala mauti chini ardhini, na tayari uharibifu umeshaingia, hapo Yesu alipomwambia Martha, “Mumemzika wapi? Na kama hutatilia shaka, utauona utukufu wa Mungu?”

<sup>59</sup> “Si nilikwambia usiwe na shaka?” Alimwambia Yairo usiku ule, au siku ile. “Kama utaamini tu, unaweza kuona utukufu wa Mungu.” Basi imani huyashinda mauti. Imani ni ushindi juu ya mauti. Imani ni ushindi juu ya dhambi. Imani ni ushindi juu ya magonjwa. Imani ni ushindi juu ya hofu. Imani ni ushindi dhidi ya misukosuko. Imani ni ushindi juu ya ulimwengu.

<sup>60</sup> Unasema, “Yohana, alipoandika hayo, hakuwa na matatizo yangu. Haikumbidi kushughulika na watu ambao ninashughulika nao. Haikumbidi kupitia mambo ninayopitia.” Hiyo ni kweli.

<sup>61</sup> Huenda haikumlazimu kushughulika na jamaa wale wale. Huenda haikumlazimu kushinda jambo lile lile. Lakini kamwe hakuyaacha nje, kwa maana alisema hivi, “Imani ni ushindi unaoushinda ulimwengu,” kitu hicho chote. Ikoje? Pata imani ndani yake. Panda juu yake. Tunapokuwa na Neno la Mungu lililoandikwa mbele zetu, na Roho Mtakatifu hapa akitenda



na kuonyesha ufufuo wa Bwana Yesu, pamoja na ahadi za Kiungu zilizoandikwa hapa, kwamba, “Chochote unachotamani unapoomba, amini kuwa umekipokea, nacho kitakuwa chako.” Inakupasa kufanya nini basi? Amini. Si imani ya kuelea tu, si imani ya kujisingizia tu, bali imani halisi.

<sup>62</sup> Sasa, imani ni mshindi. Imani ni mshindi. Sio tu mmpatanishi. Inashinda. “Imani ni ushindi unaoushinda ulimwengu.” Inafanya nini? Imani ni nini? Ni nini, “kushinda”? Kushinda na ushindi ni kitu kimoja. *Kushinda*, kunamaanisha “kupiga kabisa; kubatilisha; kutia pingu; kutupa gerezani.” Kunamaanisha kwamba dhambi iliyowahi kukutawala, unaitawala sasa. Inamaanisha kwamba umeishinda. Wewe ni. . . Umeipiga. Wewe ni mkuu kuliko ilivyo. Loo, ninajisikia wa kidini sasa hivi!

<sup>63</sup> Ni yupi aliyetangulia, mwenye dhambi au Mwokozi? Mwokozi, kwa kuwa Mwokozi ana nguvu zaidi kuliko dhambi. Ni nani aliyetangulia, mponyaji au ugonjwa. Isingeweza kuwa mponyaji isipokuwa iwe Yeye alikuwa juu ya ugonjwa. Ni mponyaji, Huyo anaweza kushinda ugonjwa.

<sup>64</sup> Nayo imani ni ushindi unaoushinda kila laana ya ibilisi. Imani ni ushindi. Imani katika nini? Si imani katika kanisa lako, si imani katika kanuni zako za imani, si imani katika mtu fulani. Lakini, imani katika Yesu Kristo Yule aliyetoa hiyo ahadi, huo ndio ushindi. Ni nini? Ni ushindi. Wasema, “Mkono wangu bado umelemaa.” Lakini imani ni ushindi. “Ningali ninajisikia mgonjwa.” Lakini imani ni ushindi. Loo, inaushinda ulimwengu.

<sup>65</sup> Unapoweza kupanda ukaingia katika Mungu, kwa maombi, mpaka uone kitu hicho kimeshindwa chini yako, hakuna kinachoweza kukudhuru basi. Umeshinda. Una maili hamsini za nafasi ya kiwiko. Unaabiri huru basi.

<sup>66</sup> Wewe ambaye umekuwa mlevi na mtumwa wa wisiki, utakuwa mtawala wake basi. Maskini ibilisi wa pombe aliyekufanya unywe pombe, ni bwana wako sasa; lakini unapopata imani, simaanishi imani ya kujisingizia, imani halisi, yeye ni mtumishi wako basi.

<sup>67</sup> Ninyi msioweza kuweka chini tumbaku, ninyi wanawake na wanaume, inapofikia mahali ambapo unaweza kufika mahali hapo, ambapo umeishinda kwa imani, utaitawala basi.

<sup>68</sup> Maskini mwanamke mmoja anayeketi hapa sasa hivi, amekuwa kwenye madhabahu hii, wakati baada ya wakati baada ya wakati. Mwanamke mzuri, lakini alianza kuvuta sigara, muda mrefu uliopita. Wala asingeweza kuishinda. Naye alikuwa amekuja huku, nami ningeomba pamoja naye, na ilionekana kana kwamba hangeweza kuishinda. Ndipo mu—muda si muda mwajua, nilimwambia hapa, nikasema, “Kutakuwa na hatari safarini.”

69 Akasema, “Ndugu Branham, nimelia, nimeomba.” Mnaona, mhemko tu, kupigana na hewa, huo hautafaa kitu.

70 Nami ningeshuka na kuomba pamoja naye, na kumwekea mikono, naye angerudi. Na—na siku chache, ningekutana naye tena, anakuangusha tu kwa moshi wa sigara, mikono ingali ya kahawia.

71 Basi usiku mmoja, huko chini, alienda kwa daktari. Alianza kuugua na kunyauka, mpaka akakonda vibaya sana. Ndipo daktari akamchunguza, akasema, “Kansa! Kuvuta sigara!” Huyo hapo, amelala hapo apate kufa, ndipo akawa makini. Mnaona? Mtu anayezama atashikilia jani. Maadamu unaweza kutoka nje ya kanisa hili usiku wa leo, unajua unaweza kwenda kujiunga na Methodistini ama Baptistini. Maadamu unaweza kuketi hapa na kusema, “Sasa nitaninii tu . . . Mimi ni mtu mzuri. Sina shida.” Naam, huwezi kujifanyia lolote. Hiyo ni kweli.

72 Lakini unapoziona dhambi zako jinsi Mungu anavyoziona, kulingana na Biblia Yake; unapooa, utatubu la sivyo uangamie. Jambo fulani litatukia. Utakuwa makini.

73 Utaondoka hapa, huku umekabwa roho yako. Daktari huko nyuma labda atainuka, aje, achunguze, aseme, “Ni mshtuko wa moyo.” Utakuwa makini.

74 Hapo ndipo ilipombidi kuwa makini. Naye mwanamke huyo ameketi, akiniangalia sasa.

75 Naye Ndugu Roberson yuko kule nyuma, na Bw. Wood hapa, Ndugu Wood anayeketi hapa mahali fulani, na mimi, tulikuwa tukishuka kwenda kuwinda, naamini, mahali fulani, kwa lori. Basi Roho Mtakatifu alionekana kutuongoza kupanda kupitia vilimani, kufikia mahali alipokuwa. Ndipo nilipofika pale, alikuwa ameota ndoto. Basi wakati Roho Mtakatifu alipoingia chumbani, naye akawa makini kweli, hakuwahi kuvuta sigara tangu wakati huo na kuendelea. Na amepata pauni nyingi za uzani, wala hawawezi kupata dalili ya hiyo kansa.

76 Ni nini? Ni imani inayoshinda. Kwa nini haikushinda nilipokuwa nikimuomba hapa? Alikuwa akipapatika tu huku na huku. Lakini daktari aliposema, “Una kansa na utakufa,” akawa makini. Hivyo ndivyo haina budi kuwa, unapokuwa makini. Kwa nini kusubiri kwa muda mrefu hivyo? Kwa nini usiwe makini sasa? Weka imani yako katika Mungu. Vipi kama mwanamke huyo angekuwa na imani kwangu? Ingeshindikana, maana mimi ni mwanadamu. Lakini alipoibadilisha imani yake, si katika Maskani ya Branham ama katika William Branham, ama katika mtu mwingine yeyote, bali akaweka imani yake katika Yesu Kristo, ndipo akapata imani. Aliinuka juu ya woga na mashaka yote, ndipo Mungu akamponya. Na, loo, yeye akashinda. Imani ni ushindi unaoshinda.

77 Mara nyingi nimeshangaa, kwa nini Wakristo wanataka kujisumbua wenyewe na mambo hayo kwa vovyote vile?

Wanaume na wanawake huja kwangu, mara nyingi, na kusema, katika maungamo yao na kadhalika, ninapofanya mahojiano hayo ya faragha, nao, tunakutana nao, tunasonga, wanaungama kuishi maisha machafu na ya ki—kila namna. Hakika, hawawezi kuyakanusha; Roho Mtakatifu yuko pale pale. Wakijaribu kulificha, Yeye huwatolea moja kwa moja. Kwa hivyo afadhali waliseme. Wakijaribu kutoka nje, Roho Mtakatifu anawazuia, akasema, “Hebu kidogo, hili hapa jambo fulani—fulani.” Kwa hiyo wanapokuja, wanaanza kuniambia kuhusu mambo madogo ya ulimwengu. Nami nayaona miongoni mwa waaminio. Unaelekea mahali fulani. Kwa nini unatangatanga? Pata shauku fulani zako. Weka lengo lako kwa Kristo, na uache kuambatana na ulimwengu.

<sup>78</sup> Utachukua gazeti, litasema, “Sasa, ati waponyaji wa Kiungu wa siku hizi? Hakuna kitu kama waponyaji wa Kiungu.” Hilo litatia shaka moyoni mwako.

<sup>79</sup> Mtu fulani anaingia kwenye redio na kusema, loo, ahubiri mahubiri mazuri sana, lakini aseme, “Siku za miujiza zimepita,” nawe utaunga hilo mkono. Unaona, hilo linakudhoofisha.

<sup>80</sup> Jisalimishe! Kuwa sawa na Mungu! Ama uwe kile ulicho, au usiwe kabisa. Endapo Biblia ya Mungu hailifundishi, basi jiepuche nalo. Kama inalifundisha, dumu Nalo.

<sup>81</sup> Inanikumbusha jambo hili. Kwa mfano, vipi kama tungefunga safari kidogo, katika siku thelathini tangu sasa, kwenda kwenye nchi nyingine? Na katika nchi hii, hali ya hewa ilikuwa nzuri sana, hata hatungerudi tena. Na huko isingetulazimu kufa wala kuzeeka, bali tungekuwa huko milele. Je, ningeweza kuwazia nikikuona ukienda kwenye duka la mali rahisi, ukinunua vikorokoro vingi kwenda navyo? Ungekuwa ukijaribu kuondoa vikorokoro ulivyo navyo.

<sup>82</sup> Na unapojihangaisha tu, kwa kujiunga na kanisa moja na kisha lingine, utajikusanyia takataka zaidi. Lakini ikiwa utatafakari unakoenda, utaondoa mashaka hayo mengi na upuuzi huo. Utakuwa na imani halisi. Ninawaambia watu. . .

“Je, wewe ni Ndugu Branham unayewaombea wagonjwa?”

“Naam.”

“Naam, hiyo ni kinyume na imani yangu.”

“Basi huna imani yoyote. Biblia inafundisha jambo hilo.”

Na sasa watu wengi huja mstarini, nao wanasema, “Vema, nina imani yote.”

“Basi unafanya nini hapa? Uh-huh. Loo, sivyo.”

<sup>83</sup> Imani halisi haijui kushindwa. Haiwezi kushindwa. Hata mauti yenyewe hayawezi kuishinda. Haijui kushindwa. Majaribu yanajua kushindwa, lakini imani haijui kushindwa. Haiwezi kushindwa. Nayoy ndiyo njia pekee unayoweza

kumpendeza Mungu. “Maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu,” ilisema Waebrania 11.

<sup>84</sup> Na katika mahali hapa, ningeweza kuwawazia mkizunguka, baadhi yenu Wakristo wanaotumia lugha chafu, kutumia maneno machafu, yasiyo na adabu, na hata hivyo uwe mfuasi wa kanisa? Je, ningeweza kukuwazia ukienda kwenye nchi nyingine, kisha ukizunguka kupitia Marekani, ukijifunza lugha yote ya mtaani ya Kimarekani uijuayo, unayoweza kusikia? Bila shaka, hungefanya hivyo. Jambo ambalo ungekuwa ukijaribu kufanya, lingekuwa ni kujifunza maneno machache ya lugha hiyo huko, hiyo ni kweli, kiasi cha kusema, “U hali gani?” kwa vyovyote vile.

<sup>85</sup> Nami nadhani inge—ingewapasa Wakristo zaidi, siku hizi, kama walikuwa wakijaribu kujifunza lugha fulani ya Mbinguni, sifa za Mungu, ambazo tutaziimba Huko, na kufurahia. Nao watu wasioamini katika kupaza sauti, ungefanya nini ukifika Kule? Ungejiona kutofaa kabisa kuwa mahali hapo. Afadhali upate imani, na ushinde sasa, kwa maana imani ndiyo ushindi ushindao. Hapana, usingekuwa ukijibandika vitu vidogo kama hivyo. Ungekuwa na ushindi.

Unasema, “Ninafanyaje hilo, Ndugu Branham?”

<sup>86</sup> Kwa nini, ni rahisi sana. Ni ninii tu... Sasa, kwenye mikutano hapa, unashangaa jinsi ya kuwasilisha hapa, jinsi... Watu walio humu jengoni, siwajui wengi, na katika mikutano yangu wakati mwingine simjui mtu yeyote, hata lugha mbali mbali. Lakini nina—ninajuaje? Ni kujisalimisha. Jitoe tu kwa Roho Mtakatifu, ndipo basi si wewe tena. Hujui utakayosema. Unamwacha tu Yeye awe ndiye anayesema. Ni rahisi sana hivi.

<sup>87</sup> Wengi wenu watu mnawaamini madaktari wenu. Na mnapaswa kuwaanini, ikiwa una daktari. Na sasa unapopata kasoro fulani, utamwendea maskini daktari huyo mwaminifu unayemwamini. Hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya. Hilo ni zuri. Ndipo basi unawasilisha kisa chako kwake. Kama akisema unapaswa kwenda hospitalini, hufanyi lolote ila kwenda nyumbani na kupakia nguo zako na kwenda hospitalini. Hakika. Unamwamini huyo daktari. Na ikiwa hataamua kuwa unataka kwenda hospitalini, au unapaswa kwenda, hasa, atakuandikia maagizo na kukupa kifurushi kizima cha vidonge. Nawe utavimeza, nawe hujui kilicho ndani ya vidonge hivyo. Lakini una imani na daktari wako.

<sup>88</sup> Vipi kuhusu Mungu? Nawe unaogopa kumeza baadhi ya Inji-li anazokupa. “Kwa kupigwa Kwake uliponywa.” “Imani ni ushindi unaoushinda ulimwengu.” Imenze uone kitakachotokea. Ni imani.

<sup>89</sup> Unaonyesha imani uliyo nayo kwa daktari wako, kwa kumeza dawa yake, ambayo hujui ni nini. Unaonyesha imani

yako kwa daktari, kwa kujisalimisha kwa upasuaji. Hiyo inathibitisha imani yako kwa huyo daktari.

<sup>90</sup> Lakini inapomfikia Kristo, unahofu kuliamini Neno Lake. Vipi basi? “Imani ni ushindi.” Ungeweza kusalimisha kisa chako kwa Yesu Kristo, usiku wa leo, kama tu vile unavyosalimisha kisa chako kwa daktari. “Nipe chochote utakacho, Bwana. Wewe ndiwe Daktari kwenye kisa hiki.” Basi umezata ushindi. Basi una imani inayoshinda. Kamwe hutatafuta mstari mwingine wa maombi. Hutawahi kutafuta kitu kingine chochote. Utakuwa nayo papo hapo. Yote yatatuliwa. Kamwe hutaruka kutoka kanisa hadi kanisa, kuona kama *hili* linayo, ama *lile* linayo, *hawana*. Umezata basi. Unapokuwa na imani, una ushindi.

<sup>91</sup> Ninawaambia kile tunachohitaji usiku wa leo Marekani, na kile tunachohitaji usiku wa leo hapa katika maskani hii, ni kumwacha Daktari Yesu aingie na kufanya upasuaji kwenye imani yetu.

<sup>92</sup> Daktari anakwambia, “Una ugonjwa kidogo wa kidole tumbo, chote kina sumu. Kinapaswa kutolewa. Una *hiki*, *kile*, ama kinginecho, ni kibaya. Kinapaswa kutolewa.” Vema, anakitoa ili mwili wako uliobaki uweze kufanya kazi ipasavyo.

<sup>93</sup> Basi imani yetu ina shida gani usiku wa leo? Tunaogopa kumwacha Mungu achukue Neno Lake la upasuaji, Kisu Chake, chenye makali kuliko upanga ukatao kuwili, na kutufanyia upasuaji, na kutwambia kwamba upuuzi wetu wa kijinga ni mbaya. Na inatupasa kufungua kila dirisha, na kusafiri kuelekea kwenye ahadi ya Milele ya Mungu. Loo, kama tutafanya hivyo, Yesu atafanya upasuaji juu ya imani yetu, akiondoa shaka lote, hofu zote, na wasiwasi wote, dhambi yote, kila kitu kilichopo. Ndipo basi imani yetu ikifanyiwa upasuaji kwa uwazi, tunatokea tukiwa kiumbe kipya. Sisi ni tofauti basi. Tunahitaji upasuaji. Je, unaweza kumwamini Yesu Kristo kwa ajili ya upasuaji huo? Je, unaweza kumwamini? Unaweza kusema, “Bwana Mungu, kwa Neno Lako?”

<sup>94</sup> “Kwa Neno Lako,” kama wanafunzi walivyosema katika Marko Mtakatifu 5. Waliposema, “Tumevuta juya usiku kucha, tusipate kitu. Hata hivyo, Bwana, kwa Neno Lako, nitashusha wavu,” alisema Petro.

<sup>95</sup> “Bwana, mimi ni mvuvi. Ninajua ishara wakati mwezi uko sawa kabisa. Ninajua wakati wanauma, na wakati hawaumi. Ninajua wanapokuwa katika makundi yao, na wakati hawapo. Isitoshe, lakini nimevuta juya usiku kucha. Na hapa kuna halmashauri ya madaktari hapa pamoja nami, madaktari wavuvi, na tunajua kazi yetu. Nasi tumetafuta kijito hiki usiku kucha, tusipate kitu. Lakini kwa Neno Lako, Bwana. Nitashusha wavu.”

<sup>96</sup> Kwa sababu M—Mpasuaji mkuu alisema hivyo! Daktari mkuu alisema hivyo! Nao wakapata samaki wengi mno nyavu

zao zikaanza kukatika. Kwa nini? Imani ni ushindi. Huenda hakukuwa na samaki hata mmoja majini. Lakini wakati Mungu ametoa ahadi, Yeye ataumba samaki na kuwaweka mle.

<sup>97</sup> Huenda ikawa huna nafasi ya kuishi. Huenda ikawa unakufa kwa kansa. Huenda ikawa umelemewa kwenye kiti cha magurudumu. Huenda ikawa u kipofu kabisa. Sijui shida yako ni nini. Lakini kama utachukua maagizo ya Daktari mkuu, “Lolote utakalo unapoomba, amini kuwa umelipokea, nalo litakuwa lako.” Na uamini ya kwamba imani hiyo itashinda magumu yoyote yaliyopo. Unaweza kulemewa sana na dhambi mpaka nafsi yako ina uchafu iwezavyo kuwa. Huenda umejaribu kuachana na hiyo hasira kali, ulimi huo unaokashifu, umbeya huo kwenye simu. Huenda ikawa umejaribu kila tiba ujuayo. Lakini kama tu utamruhusu Yesu Kristo aingie ndani yako usiku wa leo, Yeye ataifanyia imani yako upasuaji, na kukupa imani ambayo itapanda juu kupita chochote ambacho ulimwengu unaweza kutoa. Kwa nini? Imani ni ushindi unaoushinda ulimwengu.

<sup>98</sup> Unawezaje kushuku, wakati Yesu Kristo Mwana wa Mungu aliye hai yuko hapa sasa? Roho Wake Mtakatifu mkuu humu jengoni. Neno liliahidi, ya kwamba, “Tazama, nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari.” Iliahidiwa na Bwana. Mungu hana budi kutimiza Neno Lake. Je, unaamini hilo? Alipoahidi kwamba angefanya mambo haya, Mungu anawajibika kabisa kufanya hivyo.

<sup>99</sup> Sasa nawatakeni kuliwazia hilo. Endapo una dhambi, iwapo kuna kitu kibaya maishani mwako, ninawatakeni mliwazie jambo hilo, tunapoviinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu wa maombi.

<sup>100</sup> Kabla hatujaomba, ningependa kuuliza swali hili. Ningependa kuuliza kama kuna mwanamume, mwanamke, mvulana, au msichana, aliye kwenye jengo hili, ambaye angesema kwa mkono ulioinuliwa, “Bwana, inaonekana siwezi kushinda. Inaonekana ninajua kwamba sipaswi kufanya mambo haya. Na—najua sipaswi kufanya *hivi* na *vile*. Bali nataka Wewe uifanyie imani yangu upasuaji sasa hivi, baada ya Ujumbe huu. Ninataka Wewe unichunguze kikamilifu, na uufanyie upasuaji kila ugonjwa mdogo wa imani yangu, ambao ungeniua kuyashinda mambo haya.” Mwinulie mkono wako. Je, utafanya hivyo? Bwana awabariki. Mahali pamejaa mikono! Kidogo . . .

<sup>101</sup> “Na tuweke kando kila mzigo, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi, na kukimbia kwa saburi katika mashindano haya yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Mwenye kuanzisha na Mwenye kutimiza imani yetu, Bwana Yesu Kristo.”

<sup>102</sup> Ni wangapi hapa ndani, ambao ni wagonjwa na wahitaji, wangeweza kuinua mkono wako na kusema, “Bwana, ifanyie

imani yangu upasuaji. Nina haja usiku wa leo, Bwana?” Mungu akubariki.

<sup>103</sup> Imani ni ushindi. Tunapataje imani? “Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno la Mungu.”

<sup>104</sup> Sasa kwenu ninyi mlio wahitaji, nafsi yenye dhambi. Siwezi kufanya wito wa madhabahuni, kuwafanya mje hapa madhabahuni, kama mtindo wa maskani hii ulivyo, kwa sababu hakuna hata nafasi. Kuna watu waliosimama karibu na kuta. Kuna watu walio—walio huku madhabahuni hapa, na ni mahali tu ambapo hatuwezi kufanya hivyo. Lakini nitawaomba sasa. Nanyi mjitolee tu kwa Kristo kwenye saa hii tu, ninapoomba.

<sup>105</sup> Mungu Mpendwa, tungeomba rehema Zako za Kiungu juu ya watu hawa waliotubu wanaongoja ambao wanaamini kwamba Wewe uko, na huwapa thawabu wale wakutafutao kwa bidii. Nami ningekuomba uwarehemu, Bwana. Na chochote kilichopo, kansa ya mashaka, kansa ya hasira, madhara ya kutokuamini, yaondoe sasa hivi, Bwana, na uwape Roho Mtakatifu. Jaza nafsi zao kwa wema Wako. Wabatize katika ufalme Wako sasa hivi, kwa kuwa wameinua mikono yao katika kukiri imani yao. Na kukuomba Wewe, Ee Mungu wa rehema, uwafanyie haya.

<sup>106</sup> Maana wamebadili mawazo yao ya—ya kuzurura huku na huko baharini. Wanapaswa kuingia bandarini na kuchongwa na Mjenzi mkuu, na kufanywa kiumbe kipya katika Kristo Yesu, na kutiwa nguvu na Roho Wake, wakiongozwa na mapenzi Yake. Kwa hiyo uwape sasa hivi, Baba, tunapoomba kwa unyenyekevu katika Jina la Yesu, Mwanao.

<sup>107</sup> Na sasa, Bwana, kulikuweko na mikono mingi iliyoenda juu hewani, ama iliyoinuliwa hewani. Wanatambua kwamba wamekuwa mahali mahali, wengi wao. Wameendesha magari maili nyingi kuvuka ma—majimbo, kumfikia mtu fulani anayewaomba wagonjwa. Na wamekuja, labda, mbali sana huku chini. Nami kweli nathamini hilo, Bwana. Vipi kama hawakuniamini mimi, kama mtumishi Wako? Basi wasingekuja. Ninakushukuru kwa kuwaruhusu wayaamini maombi yangu.

<sup>108</sup> Bwana Mungu, ninaomba kila mmoja kwa uaminifu sasa hivi, kwamba Wewe, Mungu mkuu wa Mbinguni, utamwingiza Roho Wako Mtakatifu maishani mwao, na kukatilia mbali kila kutokuamini. Wajalie kujua kwamba, “Imani ni ushindi.” Si mtu fulani wa duniani, si kanisa fulani, ama maombi fulani kutoka kwa mtu fulani, ambayo yote husaidia, lakini imani ni ushindi.

<sup>109</sup> Tunasoma ambapo Mwanao, Mwokozi wetu, “Alikwenda katika nchi yake Mwenyewe, na kulikuwako na wale waliosema: ‘Jamaa Huyu ni nani? Huyu si ni mwana wa seremala? Hivi hatumjui Yeye pamoja na mama Yake? Na jina lake ni Mariamu. Na hawa hapa Yuda, na Yona, na dada zake.’ Nao wakachukizwa Naye. Naye akastaajabia kutokuamini kwao, wala asingeweza kufanya miujiza.”

<sup>110</sup> Tunatambua, haijalishi jinsi mtu anavyoweza kupendelewa mbele Zako, hata hivyo imani yetu wenyewe ndiyo ushindi. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utamwondosha mwanadamu katika hili, na ujionyeshe Mwenyewe hapa usiku wa leo, ambapo imani imewekwa msingi katika kanuni za ufufuo wa Bwana wetu. Yeye hajafa, lakini Yu hai hata milele. Naye alitoa ahadi, “Nitakuwa pamoja nanyi, sikuzote, hata ukamilifu wa dahari.” Nasi tunaamini ya kwamba Yeye yuko hapa.

<sup>111</sup> Nasi tunaomba, Mungu Mpendwa, ya kwamba usiku wa leo, ya kwamba Yeye atajidhihirisha wazi, kwamba yupo. Na jalia basi Roho Mtakatifu aushike kila moyo, na kuifanyia imani upasuaji, wapate kuyashinda maradhi yao, na mateso yao, na magonjwa yao. Watoke hapa wakiwa na imani iliyowekwa, haidhuru, kama hakuna jambo moja limetukia, hata hivyo itaunda imani inayosema kwamba limetendeka. Huo ndio ushindi. Huushinda ulimwengu. Kwa maana tunaomba katika Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

<sup>112</sup> Ni vigumu sana kwangu kuona jinsi ningeweza kuitisha mstari wa maombi. Kwa maana wamesongamana mlangoni hata barabarani, na hawa wamesongamana hata barabarani, na kuyazunguka madirisha, kuizunguka milango, na huku juu. Ningeweza kujaribu, ikiwa mnetaka nifanye hivyo. Ni—ningeweza kujaribu kuitisha mstari wa maombi.

<sup>113</sup> Lakini nitasema hivi, baada ya jambo hili. Nilihubiri kusadiki kwangu mwenyewe. Ninaamini, ikiwa mtakuwa na uchaji tu, na kuchukua tu imani yote mliyo nayo, kama imani ya mwanadamu, na kuikabidhi mikononi mwa Mungu, na kusema, “Sasa, Bwana, chukua kidogo changu nilicho nacho kukupa Wewe, na ujalie imani Yako inijie,” ninaamini ya kwamba atakuponya, na anijalie nikuite moja kwa moja kutoka hapa jukwaani, hata pasipo wewe kupanda hapa hata kidogo. Je, unaweza kuamini hilo? Lakini kama unayo kadi yako ya maombi, ishikilie, tutaitumia, kwa vyovyote vile. Kwa hiyo, tunaamini. Sasa, ningependa...Hilo limekuja tu sasa hivi akilini mwangu.

<sup>114</sup> Kwa maana, Billy Paul aliniambia tulipokuwa tukiingia tu, dakika chache zilizopita, angali alisambaza baadhi ya kadi za maombi usiku wa leo. Maana, tumechukua lundo kubwa jana usiku. Naye akasema, “Kulikuwa na wengine mle ndani, baba, ambao walitaka kadi za maombi. Nami nikawapa kadi za maombi.”

Nikasema, “Hiyo ni sawa.”

Akasema, “Lakini utaitishaje mstari wa maombi?”

<sup>115</sup> Wakati huo umati ulikuwa huko nyuma. Sasa wako kote pembeni. Kwa hiyo ni vigumu kupata njia ya kufanya hivyo, kufanyiza mstari wa maombi. Hatuninii. . .



<sup>116</sup> Kuna tofauti gani ya wewe kusimama hapa, au kuketi mahali ulipo? Lakini itahitaji imani fulani kufanya hivyo. Itahitaji imani yako, pamoja na imani yangu, pamoja na imani ya Mungu. Zichanganyishe pamoja, basi imani yangu na imani yako itafifia, nayo imani ya Mungu itatawala, nazo kazi zitafanywa.

<sup>117</sup> Ninataka tu kuwaulizeni jambo hili, kwa misingi hii. Je, mnaamini hili kwamba ni Neno la Mungu? Haliwezi kusema uongo, basi, kama ni Neno la Mungu. Halina budi kuwa kweli. Basi, kama ni Neno la Mungu, na ni kweli, basi Yeye anawajibika kwa kila Neno alilonena humu ndani. Anawajibika kulitimiza Neno hilo.

<sup>118</sup> Sasa, kama ulikuwa mgonjwa na ulikuwa ukifa kwa lukemia, ama kansa, ama chochote ulichokuwa nacho, kifua kikuu, nawe ukaja hapa, na kuwaleta wahudumu wote tuliowajua, humu jengoni, na kuwaleta hapa na kuwaombea, kila mmoja wenu, hata hivyo, isipokuwa wewe mwenyewe uwe na imani, haitafanya kazi. Mnaona?

<sup>119</sup> Lakini kama mtu fulani angeponywa, labda baada ya wewe kuona, ambaye aliponywa au walidai kwamba waliponywa, hiyo ingeisaidia imani yako, maana ungeona wameponywa.

<sup>120</sup> Huko Durban, Afrika Kusini, hivi majuzi, nilikuwa nikiomba nao wakamleta mtu mmoja jukwaani. Nanyi mnaijua hiyo hadithi. Nimewasimulia wengi wenu. Jinsi ambavyo mwanamke mmoja aliponywa kule, akiwa ni Mwislamu. Nao waliwaleta wengi tu kutoka kwa kila kabila. Ambapo, yapata makabila ishirini, au zaidi, yalikuwepo. Na ndipo ilipofikia mahali, kwa mvulana aliyekuwa amezaliwa, aliyeinama, akatembea kwa mikono yake.

<sup>121</sup> Ndipo wakati Roho Mtakatifu alipoanza kumwambia... Alikuwa M—Mzulu. Ndipo Roho Mtakatifu alipoanza kunena, na kumwambia mtu huyo, mhotentoti Mwafrika, hata hakujua mkono wa kulia ni upi wala wa kushoto, na hata kamwambia yeye alikuwa ni nani, wakachangamka. Na wale waganga wakasimama, wameduwa. “Kitu hiki kipya ni kipi?” wakasema. Nao machifu waliokuwa wakiyoyozewa kwa mafeni, wakayasimamisha hayo mafeni.

<sup>122</sup> Lakini alisema, “Katika kibanda chako unamoishi, kuna picha ya Bwana wangu, imetundikwa ukutani.” Nao baba na mama yake, huko nyuma kabisa, kukiwemo na mamia ya maelfu ya watu, walisimama kuishuhudia kweli.

<sup>123</sup> Naye akasema, “Sasa, kwamba, una ndugu ambaye alikuwa amepanda mbuzi wa manjano au mbwa, naye akaumiza mguu wake, na hutembea kwa gongo. Naye yuko humu mkutanoni. Lakini imani yake sasa hivi imeshinda, naye ameponywa.” Kwa sababu gani? Mshtuko huo wa mzungu, asiyeweza hata kuzungumza lugha yake, angeweza kumwambia yeye ni nani, na kilichokuwa kimetendeka. Hizo zilikuwa ni nguvu za aina gani?

<sup>124</sup> Naye huyo mvulana akasikia hayo kupitia kwa mkalimani, naye akatupilia mbali magongo yake. Naye huyu hapa anakuja, akikimbia na kuruka-ruka, kwa furaha.

<sup>125</sup> Ndipo wakati ndugu yake, ambaye asingejua mkono wa kulia wala wa kushoto ni upi, lakini alifikiria nilikuwa nikijaribu kumfanya acheze ngo-ngoma, ngoma ya kienyeji. Alipomwona ndugu yake akikimbia na kuruka-ruka, ilimfanyia jambo fulani. Basi akapita vizuizi vya dhambi vya kutokuamini. Nami nikatazama nyuma, na hilo hapo ono, lililomwambia asimame kwa miguu yake. Aliponywa.

<sup>126</sup> Naye huyo mvulana, hata pasipo na akili ya kutosha, na nia ya kutosha, kujua nilichosema, baada ya mkalimani kumwambia. Naye alikuwa na mnyororo shingoni mwake. Nami nikaushika huo mnyororo, nikasema, “Yesu Kristo anakuponya. Simama.” Huyu mvulana aliyezaliwa akiteseka, akasimama kwa miguu yake. Si hayo tu, bali akiwa na akili timamu. Machozi yakitiririka kwenye tumbo lake jeusi. Ndipo utukufu wa Mungu ukashuka mahali hapo, hata makafiri watupu elfu ishirini na tano wakaponywa kwa wakati mmoja.

<sup>127</sup> Walifanya nini? Kesho yake asubuhi, nilikuwa nimeketi dirishani, baada ya meya wa hilo jiji kuja, akasema, “Chungulia kwenye dirisha hilo. Utashangaa.” Basi kesho yake asubuhi, haya hapa malori saba makubwa ya ng’ombe yaliyojaa magongo, na viti vya magurudumu na kadhalika, yakishuka. . . Yakishuka barabarani, pamoja na watu waliokuwa ndani yao, usiku uliotangulia, wakitembea barabarani. Wazulu, na Washaghai, na Wabasato, na Wakhosa, makabila yote mbalimbali yaliyokuwa yakipigana; yalikuwa na amani, mkono kwa mkono, wakiimba, “Mambo yote yanawezekana, amini tu,” katika lugha yao ya kienyeji.

<sup>128</sup> Nilinyanyuka kutoka dirishani, na kuinua mikono yangu hewani, nikajibu tena, “Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu sauti ambayo ingemwoko mnyonge kama mimi.” Lilikuwa ni tamasha lenye utukufu ambalo haya macho yangu karibu yaone, mpaka nilipomwona Bwana katika ono, kwenye wakati huo.

<sup>129</sup> Ni nini? Inachochea kitu fulani. Watu hao hawakuwa wakielea. Ni kwamba tu hawakuwa wamesikia hapo kabla. Basi waliposikia, kwa urahisi kama wa mtoto, walilishika tu mara moja. Hamna lingine. Walininii tu. . . Hawakuhitaji kufanyiwa upasuaji wowote. Waliuona tu na kuufuatilia, nao ukawa ni wao. Hakukuwako na mtu ambaye angeweza kuwaambia vinginevyo; tayari walilionga likitukia.

<sup>130</sup> Sasa, kama Bwana Yesu angali hai, naye yuko hapa Jeffersonville, Indiana, katika Marekani hii, kama Yeye ni Mungu yeye yule tu aliyekuwa hapa hivi majuzi usiku, kuyafungua macho ya mhubiri huyo kipofu, Yeye ni Mungu yeye

yule aliyempa mtoto huyo mdogo wa lukemia, akifa, wakati madaktari kesho yake asubuhi walipomtangaza kuwa mzima.

<sup>131</sup> Hivi majuzi tu, nina makala yake papa hapa, naamini, katika mojawapo ya vitabu hivi. Sina uhakika. Nilikuwa tu nikikisoma hivi majuzi, na nadhani nilikiweka tena katika baadhi ya vitu hivi hapa. Huenda nisiwe. . . Sina uhakika. Lakini nilikuwa nikisoma makala kutoka kwa mojawapo ya ninii. . . Hii hapa, papa hapa. Moja ya magazeti hapa katika—katika Mich- . . . Ama, vema, ilikuwa kwenye uamsho wangu wa mwisho hapa juu, makala gazetini. Ambako kulikuwa na mwanamke, mimi. . . Ilikuwa huko Burlington, Vermont. Naye alikuwa amesikitika sana. Hakupata kadi ya maombi kutoka kwa hao wavulana siku hiyo. Naye Gene, na Leo, na Billy, na wengine wangukuwa hapa, waliokuwa kule. Naye alikuwa ameketi nyuma kabisa, na kwa ghafla. . . Akashangaa ni kwa nini asingeweza kuingia kwenye mstari huo wa maombi.

<sup>132</sup> Basi mtu wa kwanza akatokea, Naye akasema, “Wewe ni Bibi *Nanii*, kutoka mahali *fulani*, ndipo kitu *fulani*, kitu *fulani* kikatukia.”

<sup>133</sup> Papo hapo akavuka kizuizi hicho. Akasema, “Nilimjua mwanamke huyo. Nami najua hiyo ni kweli.”

<sup>134</sup> Mara alipowazia hilo moyoni mwake, Roho Mtakatifu mkuu akaniita huko, na kusema, “Bibi *Nanii*, anayeketi *hapa*,” huko nyuma kabisa, mara mbili ya umbali wa jengo hili. “Maskini huyo mama mwishoni, aliyevaa nguo ya kijani kibichi.” Kasema, “Wewe ni Bibi *nanii*, jina *fulani*.” Kasema, “Unasumbuliwa na kifafa. Hupata vipindi vinne au vitano kila siku.” Kisha kasema. . . Naye akaruka kwa miguu yake. Huyo alikuwa ni yeye. Na alishangaa sana, hakujua la kufanya.

<sup>135</sup> Kisha kasema, “Isitoshe, bali unasikitika sana kwa sababu mumeo yuko kwenye Hospitali ya Askari Wastaafu, na huko wameondoa karibu tumbo lake lote. Na sasa huo ugonjwa umeingia katika sehemu nyingine ya mwili wake, wala hana nafasi ya kuishi, wanasema madaktari.” Naye, huku machozi yakitiririka mashavuni mwake, kama gazeti linavyoelezea, akainua mikono yake, kwamba hiyo ilikuwa ni kweli.

<sup>136</sup> Papo hapo, katika ono, nikamwona akija nyumbani. Nami nikasema, “BWANA ASEMA HIVI. Usiwe na hofu. Atakuwa nyumbani, mzima.”

<sup>137</sup> Basi kesho yake asubuhi, alipokuwa akienda kufanyiwa uchunguzi, kwa upasuaji tena, wakati uvimbe huo mkubwa wa ugonjwa wa Limfu ulipokuwa ukipenya kwenye mwili wake. Madaktari. . . Alisema, “Hata sihisi uvimbe wowote.” Basi madaktari wakamchunguza, wasingeweza kuona uvimbe wowote. Wakamweka chini ya ekisi-rei na kufanya kila uchunguzi, naye alikuwa mzima kabisa. Ndipo akaja nyumbani kesho yake, mzima na mwenye afya.

138 Kwa nini? Imani ni ushindi. Hakuna kadi ya maombi, hakuna mikono aliyowekelewa, hakuna chochote, lakini imani ni ushindi unaoshinda yote. Hiyo ndiyo njia.

139 Mkutano wangu wa mwisho huko Chicago, kulikuwa na mama mweusi amesimama jukwaani. Ku-kunradhi, ninaamini ilikuwa ni mwanamke mzungu aliyekuwa amesimama jukwaani.

140 Basi usiku uliotangulia, maskini mwanamke wa Kiswidi alikuwepo, naye Billy akamwona akishuka chini na kuweka kiasi fulani cha pesa nyingi katika toleo kwa ajili ya Ndugu Osborn, kwa wito wake wa Afrika wa Dhahabu Nyeusi, kampeni yake. Naye Billy akaniambia, "Maskini mwanamke yule, aliyevaa lile gauni dogo la madoadoa, alipataje kiasi hicho cha pesa kuweka katika sadaka hiyo?"

141 Na kwa hiyo Billy alipoanza kutoka, alisema, "Nipe kadi ya maombi, mpenzi."

142 Kasema, "Sina zingine." Akamwendea Gene ama Leo, mmojawapo, aliyekuwa akizisambaza, na akauliza. Hawakuwa nazo tena.

143 Kwa hiyo akasema, "Dada, nitakuona kesho usiku nikupe moja."

144 Kasema, "Vema, mpenzi," naye anapanda juu kwenye roshani mahali fulani na kuketi chini. Kamwe sikujuu hilo.

145 Ndipo nilipoingia, jukwaani usiku huo, na mwanamke mmoja alikuwa jukwaani. . . Yeye alikuwa ameketi huko juu, naye akavuka kizuizi hicho, akaingia mahali ambapo Mungu alifanyia upasuaji imani yake. Hapo, alipofikia mahali hapo, Yeye alisema, "Maskini mwanamke yule anayeketi kule juu, kwenye ile roshani ya pili, mtu wa pili ndani, akiwa amevaa maskini hilo gauni dogo, la mirabamiraba, jina lake ni Bi. *Nanii*, na *nanii*. Naye anamwombea mumewe ambaye ni msimamizi wa usafirishaji kwenye reli; kiziwi katika sikio moja." Nusura azimie. Alikuwa Mlutheri. Basi alipofika nyumbani. . . Naye Bwana akasema, "BWANA ASEMA HIVI. Amepona."

146 Alipofika nyumbani usiku huo, alikuwa amesimama mlangoni, akishangilia. Na katika dakika iyo hiyo, sikio lake likafunguka, alipokuwa ameketi kitini kwenye ofisi ya msimamizi wa usafirishaji.

147 Mwanamke mweusi aliyeketi huko nje, aliona jambo hilo, akaamini. Naye alikuwa anaamini kwa ajili ya dada yake ambaye alikuwa amekaa miaka kumi katika hospitali ya magonjwa ya akili huko Little Rock, katika hospitali ya wendawazimu. Ndipo Roho Mtakatifu akamjia, na kumwambia yeye alikuwa ni nani, na dada yake alikuwa ni nani. Na kusema, "Amekuwa mwendawazimu mwenye gadhabu, akigongesha kichwa chake ukutani, kwa miaka kumi. Lakini, BWANA ASEMA HIVI, ameponywa hivi punde."

<sup>148</sup> Basi kesho yake asubuhi, walipoingia mlangoni, matroni alimkuta amesimama mlangoni, akisihi atoke nje, akiwa na akili timamu kabisa. Akatuma habari kwa dada yake, Chicago, naye akapiga mayowe. Akasema, “Mungu mwenye rehema! Hivyo ndivyo ilivyosemwa jukwaani jana usiku!” Akasema, “Mpendwa, najua huna pesa, lakini nitakutumia tiketi ya ndege upesi sana. Fika hapa. Mkutano unafunga kesho usiku.”

<sup>149</sup> Basi mwanamke ambaye alikuwa katika hospitali ya wendawazimu, miaka kumi, usiku uliofuata tu alisimama jukwaani na kumsifu Mwenyezi Mungu.

<sup>150</sup> Ilikuwa ni nini? Dada yake alipenya mahali hapo pa mambo ya ulimwengu. Mambo ya ulimwengu hayamaanishi tu kuvuta sigara, na kunywa pombe, na kufanya maonyesho. Yanamaanisha kutokuamini. Alipitia hayo yote, mpaka akagundua kwamba imani yake inashinda. Akasema, “Kama Mungu anaweza kufanya hivyo kwa ajili ya mwanamke huyo mzungu, Mungu anaweza kufanya hivyo kwa ajili yangu, mwanamke mweusi.”

<sup>151</sup> Mungu alifanya hivyo. Na Mungu atafanya hivyo kila wakati imani yetu inaposhinda shaka, haijalishi ni mbaya kiasi gani. Loo, Yeye yu hai!

<sup>152</sup> Je, kuna watu wowote hapa ambao ilitokea walikuwa Chicago usiku huo, waliomsikia huyo mwanamke akishuhudia? Inueni mikono yenu. Vema, naam, angalia pande zote hapa. Hakika, alikuwa pale, mwanamke ambaye alikuwa hospitalini miaka hii yote.

Ni nini? Imani ni ushindi.

<sup>153</sup> Sasa, Yesu yeye yule yuko hapa usiku wa leo. Basi, kama ninaweza kuiachilia imani yangu, kwa ahadi Yake, basi Yeye atarudi moja kwa moja na kufanya jambo lile lile, kama unaweza kuiachilia imani *yako* kwenye ahadi.

<sup>154</sup> Kama atamfanyia yeyote wenu mnaoketi huko nje kwenye kusanyiko hilo, je, mtaamini Yeye angali hai? Je, hivyo ndivyo alivyofanya alipokuwa duniani? Je, hivyo ndivyo mitume walivyofanya? Paulo alimtazama mtu huyo, na kadhalika. Na huku Yesu akimwambia yule mwanamke kisimani.

<sup>155</sup> Yule mwanamke alipoligusa vazi Lake, akatoka nje na kuketi, Yeye aligeuka, akasema, “Ni nani aliyenigusa Mimi?” Hakujuua ni nani aliyemgusa, kwa hivyo akasema, “Ni nani aliyenigusa Mimi?” Wote wakakana. Akasema, “Lakini nimekuwa dhaifu. Nguvu zimenitoka.”

<sup>156</sup> Naye akatazama huku na huku mpaka akamwona yule mwanamke aliyekuwa amefanya jambo hilo. Alikuwa anatokwa na damu. Akamwambia, “Imani yako imepata ushindi.” Ni nini? Kamwe hakusema, “Nilikuponya.” Alisema, “Imani yako

imekuokoa. Ulifanya nini? Ulikuwa na imani inayoshinda, iliyotiisha, iliyokanyagia chini kila shaka.”

<sup>157</sup> “Maana alisema moyoni mwake, ‘Kama nikiweza kugusa vazi Lake, nitapona.’” Yesu alikuwa . . . Ilibidi achukue hiyo kwa jambo fulani alilowazia niani mwake.

<sup>158</sup> Hili hapa Neno Lake Mwenyewe, kudai ya kwamba Yeye angekuwa hapa siku hizi na kufanya lile lile alilofanya wakati huo. “Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo ninyi mtaniona. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, hata nyingi kuliko hizi mtazifanya. Ninaenda kwa Baba Yangu, nanyi mtafanya nyingi kuliko hizi.” Hili hapa. Tunaishi katika siku hii ya mwisho. Yesu yuko hapa.

Hebu tuombe, na tuamini. Nanyi aminini wakati nikiomba.

<sup>159</sup> Bwana, hili hapa kundi la watu. Nawe ni Mungu mkuu. Tunaona katika Biblia, ambapo uliwaponya makutano. Ambapo katika safari ya Israeli, Musa, walipotoka nyikani, hapakuwa na mtu mmoja dhaifu kati yao. Wewe ni Daktari mkuu. Wewe ndiye Daktari mkuu wa upasuaji. Na sasa, Bwana, jalia watu hawa walio wagonjwa hapa usiku wa leo, katika miili yao ama katika nafsi zao, kwamba sasa hivi wakikabidhi kisa chao mikononi Mwako, yule Tabibu mkuu. Nawe uwafanyie upasuaji, Baba, kiasi kwamba mashaka yao yote yangeondolewa. Sasa, Neno Lako lilisema ya kwamba Wewe ni “yeye yule jana, leo, na hata milele.” Tunakuomba utumie hicho kama kisu, na ukishushe kisu hicho na kujitangaza Mwenyewe kuwa ni yeye yule. “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu.” Halafu basi, Bwana, watu watakapoona ya kwamba Wewe uko hapa, imani yao na ipande juu ya kila ugonjwa ulioko katika hili jengo, wa dhambi au magonjwa, na waponywe. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>160</sup> Je, mnaweza kutambua au kuthamini mahali linaponiweka? Sasa angalieni hapa. Kuna angalau watu mia mbili na hamsini wamesimama hapa, ama zaidi ya hao, nadhani. Naam, nadhani kuna zaidi. Si—sijui. Lakini kuna wengi wenu nisiowajua. Ni wangapi hapa hawajui. . . Unajua kuwa sikujui wala sijui una shida gani? Inua mkono wako. Naam, bwana. Vema, kunao, kila mahali. Hakika. Siwajui, lakini Yeye anawajua.

<sup>161</sup> Sasa, kama Yeye ataninii . . . kama utajisalimisha tu Kwake na umwache aseme nawe kwa imani ile ile aliyokuwa nayo yule mwanamke, utamwamini? Kama—kama ni . . . Kama jambo lolote ni ukweli uliohibitishwa, ni ukweli uliohibitishwa.

<sup>162</sup> Kama mtu akishuka hapa na kusema, “Nina tiba ya kansa.” Alichukua kansa hapa nje, iliyokuwa ikiingia katika hali mbaya, na kuwachukua madaktari huko chini na kuwathibitishia ya kwamba kansa inaweza kuponywa, kila mtu ulimwenguni angeikimbilia hiyo, tiba hiyo.

163 Mbona, ndugu, nimemwona Yesu Kristo akitibu kansa nyingi sana! Lakini, hata hivyo, Yeye anauliza jambo moja tu, “Ikiwa utaamini.” Hilo linaonekana kuwa ndilo jambo gumu kuliko yote. Nimemwona akifungua macho ya vipofu, akiwafanya viwete kutembea. Nimemwona akiwafufua wafu, wakiisha kufa, wametangazwa na daktari. Mambo mengi sana, ingechukua. . . Nisingeweza kuandika majuzuu ya vitabu, kuelezea kile ambacho nimemwona akifanya, mimi mwenyewe. Na bado ni ngumu sana, kupata kuamini.

164 Sasa ikiwa ninyi nyote wagonjwa humu ndani. . . Nawatakeni kila mtu awe na uchaji awezavyo. Sasa, naamini. . .

165 Mimi ni mwaminio mkubwa wa mhemko. Ninaamini, chochote kisicho na mhemko kimekufa. Kama dini yako haina mhemko kidogo juu yake, afadhali uizike. Maana. . . Lakini kuna nyakati za mambo yote.

166 Ukinijia mimi, na ningeweza kukupa. Na kusema, “Ndugu Branham, nataka dola mia moja.” Ungekuja kwa heshima sana, na kusema, “Ndugu Branham, nina haja sana ya dola mia moja.” Na—nawe unajua nilikuwa na dola mia moja mfukoni mwangu, na unaamini kwamba kwa ninii yangu. . . nikitumia huruma yangu, kwamba ningekupa hizo dola mia moja. Vema, sasa, ungesimama hapo kwa uchaji, ukitarajia kuzipokea.

167 Ndipo nilipokupa hizo dola mia moja, ungeweza tu kupiga mayowe kwa sauti kubwa ulivyotaka. Una dola mia moja mkononi mwako. Unaona?

168 Sasa, lakini, unapokuja, njoo kwa heshima. Usije, ukipiga mayowe, na kuniomba hizo dola mia moja; huenda nisikuelewe. Unaona? Lakini njoo, uniombe. Ndipo nikikupa hizo dola mia moja, basi anza kupiga mayowe. Kwa hiyo wakati. . .

169 Hebu tumjia Mungu na kumwomba ampeleke Roho Wake Mtakatifu, ndani ya kuta au nje ya kuta, popote pale. Sijali umesimama wapi. Popote pale, sijali. Kama ni nchini kote, nawe unamwomba mtu fulani, Yeye atamleta. Basi hebu tuone.

170 Mungu alisema, “Nithibitisheni Mimi.” Hiyo ni njia nzuri ya kuthibitisha kama Mungu ni Mungu, au la. “Nithibitisheni Mimi,” asema Bwana.

171 Sasa, kama Yeye ni Mungu, basi, na tunajua ndivyo alivyo, hebu na tumwombe afanye mambo hapa, usiku wa leo, aliyofanya, na ndipo hutalazimika kuja hapa juu. Na kama itafanywa, angalau watu watatu tofauti, kote humu jengoni, kama ikitokea, kama itawagusa watu ninaowajua, si—sitaki kumkubali huyo kama mmoja, mnaona, ninalitaka hivyo, kwa mtu ambaye simjui.

172 Sasa, kuhusu kuyajua magonjwa, kuna mtu mmoja tu hapa ndani, ninayemjua, kwa ugonjwa wowote; na huo sio ugonjwa. Huyo ni maskini rafiki yangu mwema, na wa kupendeza,

Edith Wright, anayeketi kule nyuma. Ninamfahamu. Alikuwa ameteseka kwa miaka kadhaa. Tulimwombea, wala kamwe. . . Maumivu yakaisha basi, yamekwisha kwa muda mrefu. Lakini Bwana hajapata kumkomboa huyu msichana kutoka kwa mateso yake. Ninajua tatizo la Edith. Nje ya huyo, sijui mtu yeyote humu ndani, una ugonjwa gani.

<sup>173</sup> Lakini ikiwa unanijua, basi a—afadhali iwe hivyo, ili kwamba uone ya kwamba si mimi, ya kwamba ni Bwana.

Sasa wewe omba. Nitaomba. Na tumwamini tu Bwana.

<sup>174</sup> Na sasa, Dada Gertie, polepole tu uwezavyo, nataka ucheze, “Tabibu mkuu sasa yu karibu, Yesu mwenye huruma.”

<sup>175</sup> Ninatazama huku kwa Ndugu Banks Wood, rafiki yangu. Yeyote anajua, anayemjua Ndugu Wood hapa maskanini, yeye ni mmoja wa wadhamini hapa. Lakini hapo awali alikuwa Shahidi wa Yehova. Hili hakika lilikuwa ni jambo kubwa kwake, lakini, alipokuja Louisville na kumwona Bwana akifanya jambo fulani. . . Alikuwa na mvulana aliyelemaa, kitu kama polio kilikuwa kimeupinda mguu wake kabisa. Naye aliifuatilia hiyo mikutano. Sikujua. Sikuwahi kusikia habari zake. Lakini alipopanda kuja hapa kwenye. . . Mahali fulani, nilirudi kutoka nchi za ng’ambo, kutoka Uswidi, akiwa ameketi kule nyuma kabisa jengoni, usiku huo, Bwana Yesu akamwita mvulana huyo, David, na kumponya. Na leo hii, mvulana huyo karibu hajui ni mguu gani, ulioponywa. Unaona?

Loo, mamia ya mambo! Ikiwa tu utaamini!

<sup>176</sup> Sasa, wakati mmoja ninaoweza kukumbuka, na kwa kweli niliombea hilo. Nakumbuka, ilikuwa. . . Ninaona baadhi ya Waamishi, naamini, ama labda Wamenoni, mojawapo, jengoni, na maskini wasichana wamevaa kofia zao ndogo. Hao ndio tu walionifanya niwazie hilo. Nilikuwa huko Fort Wayne, Indiana. Na kulikuwa na maskini msichana wa Menoni ambaye alikuwa amempokea Roho Mtakatifu. Au, inawezekana alikuwa Muamishi. Ilikuwa ni mojawapo, mmoja wa watu hao, ama Mmenoni au Muamishi. Naye alikuwa m—msichana mzuri sana. Naye alikuwa akicheza, “Tabibu mkuu sasa yuko karibu, Yesu mwenye huruma.”

<sup>177</sup> Basi kulikuwa na m—mtoto mchanga aliyekuwa ameletwa mikononi mwangu, alikuwa amelemaa. Ndipo nilipoomba, huyo mtoto mchanga aliponywa. Akaruka kutoka mikononi mwangu na kukimbia chini jukwaani. Naye mama yake akazimia.

<sup>178</sup> Naye huyo msichana wa Kiamishi au Mmenoni alimjua huyo mama. Naye. . . Roho Mtakatifu akamgusa naye akaanza kupiga makelele. Ndipo akainua mikono yake na kukimbia kutoka kwenye hiyo piano.

<sup>179</sup> Nayo piano haikukosa sauti hata moja, ikicheza, “Tabibu mkuu sasa yuko karibu, Yesu mwenye huruma.” Huku



wakishuka kupitia marefu hayo ya kanisa, kutoka kila mahali, watu walikuwa wakisongamana wao kwa wao. Navyo hivyo vibao vya pembe za ndovu vikienda juu chini, “Tabibu mkuu sasa yuko karibu, Yesu mwenye huruma.” Nao wamelala sakafuni, kwenye marefu ya kanisa, wamelemewa na—na hofu, au, wa, au, uwepo wa Roho Mtakatifu.

Yeye angali hai. Angali ni Yesu.

180 Sasa hebu tuuvumishe huo kimya kimya kwa dakika moja tu. Kisha sisi . . . ndipo tutaona yale Bwana anayosema. Kila mtu sasa jiweke kwenye imani. Anzeni kuangalia huku, na muamini kwa moyo wenu wote.

Tabibu mkuu yu karibu sasa,

181 Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utafunua yale yaliyo katika mioyo hii. Katika Jina la Yesu.

. . . kufurahisha moyo,  
Loo, isikieni Sauti ya Yesu.

Sauti nzuri sana katika wimbo wa serafi,  
Jina tamu sana . . .

182 Sasa ninyi wagonjwa anzeni tu kuondoa mashaka yote. Wengi wenu hamjawahi kuona hii awali. Semeni, “Ninaamini, kwa vyovyote vile.”

Yesu, Yesu wa thamani.

183 [Ndugu Branham anavumisha *Tabibu Mkuu*, kisha anatulia kwa sekunde thelathini—Mh.]

184 Natumai mimi sio mlokole. Lakini inaonekana kwangu sasa kama tu ninaingia chumbani kwangu, navuta mlango pamoja, naingia katika chumba cha siri na kufunga milango. Ninalifungia nje tu kusanyiko lote kutoka pande zote sasa, mnaona. “Na kumwomba Baba yenu aonaye kwa siri, na Yeye aonaye kwa siri atakujazi hadharani. Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, mtapata; bisheni, itafunguliwa; kwa maana kila atafutaye hupata.”

185 Hebu mwazie Yeye akiwa hapa sasa. Yule unayemwona kwenye picha pale, ile Nuru, ile Duara ya Nuru, haiko mbali. Ni mpambanuzi wa mawazo. Ni Kristo. “Muda kidogo . . . Natoka kwa Mungu, nami nitarudi kwa Mungu.” Alirudi. Akarudi moja kwa moja kwenye kile Yeye alichokuwa. Atakapokuja tena, atakuwa katika mwili wa nyama kama alivyokuwa, Bwana Yesu.

186 Unaweza kusema, “Ndugu Branham, unafanya nini?” Ni kujisalimisha tu. Sasa hilo . . . Nimesimama tu hapa.

187 Haya si maonyesho sasa. La, bwana. Msiwazie hilo, mtakuwa kwenye misingi mibaya.

188 Anajaribu, anajaribu kujipenyeza mahali fulani. Neno la Mungu liko hatarini. Nimesema kwamba alikuwa. Vipi kama sivyo? Yeye daima atalitimiza Neno Lake. Siogopi hilo.

189 Mtu fulani, mahali fulani, ataushika upindo huo wa vazi Lake. Biblia ilisema, “Yeye sasa,” sasa hivi, “ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.”

190 Unaniangalia kwa uaminifu sana, mama, unayeketi hapo umevaa hilo gauni la bluu. Sikujui, sidhani. Inaonekana siwezi kupata mawasiliano popote na imani ya mtu. Labda ingesaidia. Je, una haja na Mungu? Kama hatufahamiani, inua mkono wako. [Dada huyo anasema, “Sidhani unanijua, Ndugu Branham, bali ninakujua mimi.”—Mh.] Sikujui, lakini unanijua. Vema. Sina fununu ya kilichokuleta hapa. Sijawahi kukuona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Labda umekuwa kwenye mkutano wangu mahali fulani. Kama Bwana Yesu ataniambia shida yako ni nini, ungeamini? Itakubidi kuamini kama ni ukweli. Na labda hiyo itawapa wengine imani, kuanza kutenda kazi, unaona. Sijui. Nimekuona tu umeketi pale ukinitazama. Karibu hujayaondoa macho yako kwangu. Uko karibu.

191 Mwanamke huyu anayeketi mbele hapa, namfahamu. Watu hawa *hapa*, najua.

192 Sikufikiri nilikujua. Sikujui, lakini Yeye anakujua. Na kama una haja, kama vile tu ulivyokuwa umesimama hapa jukwaani.

193 Naam. Sasa mtu yeyote anaweza kuona. Natumaini unaweza. Inaonekana kwangu, ya kwamba, huyu mwanamke anafifia sana. Lakini ana jambo jingine kasoro. Ana ugonjwa wa ngozi. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Uko mwilini mwake ambao hauonyeshi, lakini anao. Hiyo ni sahihi. Mnaona, mawasiliano tu.

194 Wakati, “Yeye alisema, ‘Tutazame sisi.’ Na wakati walipomkazia macho, Paulo akasema, ‘Ninaona kwamba una imani ya kuponywa.’”

195 Vipi kuhusu maskini mama huyo anayeketi karibu nawe? Kwa namna fulani ilipenya kizuizi, ikaja kwake, kwa maana alikuwa akiomba pia. Sikujui wewe. Hatufahamiani. Hiyo ni kweli. Ikiwa Roho Mtakatifu atanifunulia shida yako ni nini au uko hapa kwa sababu gani, au kitu fulani katika maisha yako ambacho unajua sijui, utaamini kuwa ni . . . kwamba Nguvu hizo, Nguvu zisizoonekana, zinatoka kwa Kristo? Nataka kukuuliza jambo fulani. Sasa hivi, una hisia juu yako, hisia tamu sana, tulivu, nyenyekevu. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mnaona? Ndivyo ilivyo. Papo hapo juu yako inasimama Nuru ile. Nawe unasumbuliwa na shida kutoka kwa miguu na nyayo za miguu yako. Hiyo ni kweli. Sivyo? Watikisie watu leso hiyo, kama hiyo ni kweli, ili waone. Sidhani kama utawahi kusumbuliwa nayo tena. Hiyo ni . . .

196 Ni nini kinachofanya hivyo? Nini . . . Hao hapo watu ambao sijawahi kuwaona maishani mwangu. Ni nini kinachofanya hivyo? Hao ni wawili.

197 Kuna kijana anayeketi papo hapo karibu na mwanamke huyo, papo hapo sasa. Naye alianza kulia mara Hiyo ilipopiga. Ni kitu fulani kuhusu mwanamke huyo. . . Hapana. Ni huyo kijana mwanamume, mwenyewe. Anasumbuliwa na koo lake na kichwa. Hiyo ni kweli. Ninaamini hatufahamiani, ewe kijana mwanamume. Sijawahi kukuona. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, inua mikono yako.

198 Hao hapo watu watatu, wameketi katika safu moja. Sijawahi kuwaona, sijawasiliana, maishani mwangu, na watu hao. Je, mtaamini?

199 Mtu fulani upande *huu* sasa, aliye *hapa* ndani. Ni wangapi walio wagonjwa na wahitaji, upande huu? Inueni mikono yenu, kila mmoja upande huu, ambaye ni mhitaji. Loo, ni kila mahali. Vema. Sasa endeleeni tu kuamini.

200 Mtu huyu anayeketi, akiniangalia, huna budi kumpata Kristo la sivyo utakufa. Kansa ingekuua. Mungu ndiye mponyaji.

201 Huyu bi kizee anayeketi *hapa*, papa hapa kitini. Anasumbuliwa na ugonjwa wa tumbo na yabisi kavu. Hiyo ni kweli. Unaamini kuwa imetimizwa?

202 Wewe unayemtazama mahali alipo. Unaamini? Je, unamhitaji Kristo? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Kivimbe hicho unachotaka kiondolewe, unaamini Mungu atakiondoa? Siuoni huo uvimbe, lakini upo. Upo shingoni mwako, upande wa nyuma. Labda nikikwambia jina lako ni Bi. Welsh, ungeniamini basi? Sivyo? Hiyo ni kweli. Sivyo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo, ni kweli."—Mh.] Vema. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Unajua hilo. Uh-huh. Unamwamini Mungu.

203 Kuna ishara ya mauti juu ya maskini mwanamke anayeketi hapo, kansa, pia. Unaamini, mama, ya kwamba Mungu atakuponya? Unaamini? Unaugua kansa. Ni kivuli cheusi kinachoning'inia juu yako. Nakwambia sasa, kimeondoka, kama utaamini.

204 Simjui mwanamke huyo. Sijawahi kumuona maishani mwangu. Sijui hata mmoja wa watu hawa, ni juavyo mimi. Mtaamini?

205 Ninamtazama mwanaume. Sidhani kama nimewahi kumwona hapo awali, maishani mwangu. Anasumbuliwa na ngiri. Unaamini Bwana atakuponya, bwana, hiyo ngiri, akupe afya? Mke wako ana wasiwasi na udhaifu. Kasisi Reed, hilo ndilo jina lako. Sikujui wewe. Wewe si wa nchi hii, kwa vyovyote vile. Umetoka Ohio. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inuka. Yote yamekwisha sasa, kwako na kwa mke wako, nyote wawili.

Amiini kwa moyo wako wote. Je, unaweza kuamini sasa?

206 Huko nyuma kabisa kwenye mstari huu, nyuma kuelekea upande *huu*, je, hamwezi kuiona hiyo Nuru ikining'inia pale pale? Ni mwanamke anayesumbuliwa na maambukizi ya virusi, moja kwa moja kwenye mstari huu hapa. Wewe hutoki kwenye mji huu. Umetoka mahali paitwapo Columbus, Indiana. Jina lako ni Elisabeth. Unaishi kwenye barabara inayoitwa Barabara ya Ohio. Nambari yako ni 1932 Barabara ya Ohio. Nenda, amini. Umekuacha sasa. Amini.

207 Na sasa huyo Roho anajongea. Anaenda *hivi*, *hapa*, kwa mwanamume fulani. Na ni uhusiano fulani. Hapana. Ni, anatoka Columbus. Naye anaumwa na jicho na ki—kidonda. Unaamini Bwana Yesu atakuponya, bwana, akupe afya? Na maskini mpwa wako aliyeketi mbele yako hapa, mtoto wa dada yako, alikuwa na aina fulani ya ugonjwa wa mifupa, wala hatakula sasa. Inafanya kitu kama kinyongo kwake. Ikiwa utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuponywa. Mwamini Mungu.

208 Ni wangapi wenu wanaoamini sasa?

209 Ninaona kivuli kingine cha kansa kimeketi pale. Kama utaamini kwa moyo wako wote, dada, itakwisha. Unaweza. . .

210 Je, imani yako imepita mstari huo wa mashaka sasa? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba imani yenu imepita mstari wa mashaka? Inua mkono wako. Basi ni nini kilichosalia ila kuwa huru? Yote yamekwisha.

211 Wasichana hawa wadogo wanaoketi hapa kitini, ninawajua. Sikuwajua ninyi kuanzia jana usiku, lakini ninawajua sasa. Nilisikia habari zenu, leo hii, kutoka kwa mke wangu. Jina la mama yenu lilikuwa Fulkerson kabla ya kuolewa. Na huo ni ugonjwa ambao hakuna mtu anayejua chochote kuuhusu. Vidole vyenu vinashikwa tu na maambukizi, na mnashikwa na kitu kama ugonjwa wa damu, au kitu fulani mikononi mwenu, na muda si muda mwajua, vidole vinatoka, na kadhalika. Ninyi nyote wasichana wawili wadogo. Ninyi ni wasichana wawili warembo. Namjua mama yenu. Bibi yenu aliponywa usiku mmoja nilipomwendea, miaka ishirini na kitu iliyopita, akiwa na TB. Hiyo ni kweli. Bi. Fulkerson.

212 Mungu amkemei ibilisi huyo anayewazuia ninyi wasichana wadogo warembo! Nguvu zilizomfua Yesu kutoka kaburini, na zitupilie mbali kitu hicho, kisiwasumbue tena. Ninasema hivyo kwa mamlaka ya Neno la Mungu. Huna budi kumkasirikia ibilisi.

213 Mungu hutupa ushindi. Tunao sasa hivi. “Huu ndio ushindi uushindao ulimwengu, hiyo imani yenu.”

214 Ninyi nyote mnaoamini kwamba mmeponywa na Nguvu Zake, simameni kwa miguu yenu na mumpe Yeye sifa, kila mahali jengoni. Inueni mikono yenu sasa na hebu tumsifu Yeye.

<sup>215</sup> Asante, Bwana Yesu, kwa nguvu Zako za uponyaji. “Hii ndiyo imani ishindayo. Huu ndio ushindi, imani yetu.” Sasa tunawatangaza wameponywa, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Tujalie, Bwana.

*Nitamsifu, Gertie. Nitamsifu.*

<sup>216</sup> Je, umepita mstari wa kizuizi?

Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili  
ya wenye dhambi;  
Mpeni utukufu, enyi watu wote,  
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

Vema, njoo pamoja nao sasa.

Nitamsifu, nitamsifu,  
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili  
ya wenye dhambi;  
Mpeni utukufu, enyi watu wote,  
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

<sup>217</sup> Sikilizeni. Ningali ninaamini, marafiki, kwamba hamwezi kupanda mwingie mahali pale. Sitamruhusu ibilisi aushinde mkutano wa aina hii. Hakuna sababu yake. Injili imehubiriwa, naye Kristo yuko hapa kuithibitisha. Ibilisi ni mwongo. Ninyi, kila mmoja, mmeponywa na Yesu Kristo. Kazeni mwendo na imani hiyo hapo. Hiyo hapo. Ni yako. Usielee tena. Imarishwa pale Kalvari, na umpe sifa na utukufu. Mwambie unampenda. Mwambie unamthamini. Na uupitie huo mstari wa utengano, naye Mungu atakuponya na kukupa afya. Kweli limaanishe. Usiseme tu. Limaanishe kutoka moyoni mwako, na umpe sifa.

Nitamsifu,

Kutoka moyoni mwako sasa, juu kabisa!

. . . nitamsifu,  
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili  
ya wenye dhambi;  
Mpeni utukufu, enyi watu wote,

Mpeni sifa!

Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

<sup>218</sup> Ni aina gani ya doa? Doa la shaka. “Sasa nimeponywa. Kwa kupigwa kwake nimeponywa. Mimi ni mali ya Bwana. Magonjwa yangu yametoweka. Nitamsifu. Nitamsifu. Nitampa utukufu. Nitapiga kelele za ushindi. Nitamwambia nampenda. Ninamwamini. Niko huru.” Haleluya!

. . . watu,  
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.  
Nitamsifu, nitamsifu,  
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili  
ya wenye dhambi;  
Mpeni utukufu, enyi watu wote,

Kwa kuwa Damu Yake imeosha . . . (Ndiyo hiyo.  
Penya uingie ndani yake!) . . . kila doa.

Nitamsifu, ni- . . . (Haleluya! Haleluya!)  
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili  
ya wenye dhambi;

Mpeni utukufu, enyi watu wote,  
Kwa . . . (Ndiyo hiyo!) . . . imeosha kila doa.

Nitamsifu, (Kuoshwa tu kwa Damu  
daima!) . . . Yeye,

Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili  
ya wenye dhambi;

Mpeni utukufu, enyi watu wote,  
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

<sup>219</sup> Utukufu! Bwana asifiwe! Mnampenda? Msifuni! Msifuni!  
Kristo mtukufu! Mungu Mtukufu, anayeishi milele sasa! Yehova  
Mungu wa Agano la Kale, aliyepo katika siku hizi! “Jinsi kazi  
Zake zilivyo za ajabu na za kushangaza!” “Ishara Zake na  
maajabu hayachunguziki.” Loo, ni ajabu jinsi gani! Loo, Yeye  
ni mtukufu!

<sup>220</sup> Ni wangapi wenu wanaohisi Uwepo wa Mungu sasa  
hivi? Hakika! Sasa acha kila shaka litoweke kutoka kwenu.  
Mmeponywa. Kwa kupigwa Kwake mmeponywa. Imekwisha.  
Msifuni na mume utukufu!

<sup>221</sup> Roho Mtakatifu, akishuka pande zote humu jengoni! Ile  
Duara kuu ya Nuru, ikizunguka mahali hapa! Ni ajabu jinsi  
gani! Jinsi tunavyompenda!

Basi vita vitakapokwisha, tutavikwa taji!  
Naam, tutavikwa taji! Naam, tutavikwa taji!

Basi vita vitakapokwisha, tutavikwa taji  
Katika Yerusalemu mpya.

Tutavikwa taji, tutavikwa taji,  
Tutavikwa taji angavu na ing'aayo.

Basi vita vitakapokwisha, tutavikwa taji  
Katika Yerusalemu mpya.

Tutavikwa taji, tutavikwa taji,  
Tutavikwa taji angavu na ing'aayo.

Basi vita vitakapokwisha, tutavikwa taji  
Katika Yerusalemu mpya.

<sup>222</sup> Hii, kwa maoni yangu, ni kama tu Roho Mtakatifu  
aliyeshuka Siku ya Pentekoste, ambaye alizikata pingu.

<sup>223</sup> Ilitokea tu nimemwona, ndugu Mmenoni amesimama  
hapa mkutanoni. Huko Indianapolis, aliingia, naye alikuwa  
akishikwa na kifafa kwa miaka mingi, mingi sana. Naye Roho  
Mtakatifu akamwita, mkutanoni, naamini ndivyo ilivyokuwa.  
Na hajawahi kamwe kuanguka tena. Bwana Mungu alimponya  
na kumfanya mkamilifu, mzima; mhubiri Mmenoni.

<sup>224</sup> Loo, si Yeye ni wa ajabu! Hakuna ajuaye, kwa wale ambao wameonja wema Wake, wanajua jinsi alivyo mwema!

<sup>225</sup> Sasa, marafiki, nionavyo mimi, hii ndiyo ile dini ya kale, wakati Bwana Yesu Kristo anapokuja miongoni mwetu na kutubariki. Tuna furaha sana uko hapa. Ninaamini ya kwamba kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu ni, sasa hivi, kama imani yako imezamishwa na mashaka yote yako huko nyuma, uko huru sasa. Usidai kamwe ugonjwa wowote, kuanzia sasa na kuendelea. Endelea. Ulikabidhi kisa chako kwa daktari mmoja; mkabidhi Yesu sasa. Amekufanyia upasuaji na kuondoa shaka lote, ili uweze kuipata. Bwana akubariki.


Ni ile dini ya zamani,  
Nayo ni nzuri vya kutosha kwangu.

Ni ile dini ya zamani,  
Ni ile dini ya zamani,  
Ni ile dini ya zamani,  
Nayo ni nzuri vya kutosha kwangu.

Hunifanya nimpende kila mtu,  
Hunifanya nimpende kila mtu,  
Hunifanya nimpende kila mtu,  
Nayo ni nzuri vya kutosha kwangu.

Loo, ni ile dini ya zamani,  
Ni ile dini ya zamani,  
Ni ile dini ya zamani,  
Nayo ni nzuri vya kutosha kwangu.

. . . ninapokufa,  
Itafaa ninapokufa,  
Itafaa ninapokufa,  
Nayo ni nzuri vya kutosha kwangu.

Ni ile dini ya zamani,  
Ni ile dini ya zamani,  
Ni ile dini ya zamani,  
Ni nzuri vya kutosha kwangu. 

58-1004 Imani Ndiyo Ushindi Wetu  
Branham Tabernacle  
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)



## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)